**102/1**

**KISWAHILI**

**KARATASI YA KWANZA**

**INSHA**

**JULAI/AGOSTI 2018**

**MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA PILI**
**KIDATO CHA NNE**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. **Sura**
   (i) Insha iwe na kichwa
   (ii) Iwe na tarehe
   (iii) Iwe na utangulizi
   (iv) Iwe na mwili na maelezo kiaya
   (v) Yaweza kuwa na maoni au msimamo wa mhariri.
   (vi) Iwe na hitimisho – Jina la mhariri na wadhifa wake.

**Maudhui**

(i) Kupiga vita ndoa za mapema.
(ii) Kupiga marufuku ajira ya watoto
(iii) Wasichana kupewa nafasi ya kuendelea na masomo baada ya kujifungua.
(iv) Alama za kujiunga na shule na vyuo kupunguzwa.
(v) Elimu bila malipo kwa shule za msingi na vyuo.
(vi) Kutoa msaada wa karo kwa familia maskini
(vii) Kujenga shuleni zaidi za wasichana.
(viii) Kupanua shule za wasichana zilizoko.
(ix) Kuhamasisha wazazi kuhusu umuhimu wa elimu ya msichana.
(x) Adhabu kali kwa wabakaji
(xi) Kutoa sodo kwa wasichana shuleni.
(xii) Adhabu kali kwa wanaoshiriki ukeketaji

2. Hili ni swali la mjadala
   - mtahiniwa atoe hoja za kuunga na kupinga.

**Kuunga**

(i) Nchi kupunguza madeni.
(ii) Kuzuia nchi kufilisika
(iii) Kuzuia mfumko wa bei.
(iv) Kupunguza tofauti ya kimapato ya wafanyikazi wake.
(v) Kuboresha uchumi wa nchi.

**Kupinga**

(i) Ni kinyume na haki za wafanyikazi.
(ii) Viwango vya ufisadi kuongezeka.
(iii) Motisha ya wafanyikazi kupungua.
(iv) Kugura na kujiunga na sekta ya kibinafsi kwa wataalamu.
(v) Uwezekaji kupungua kutokana na uchechefu wa fedha.
(vi) Kuhamia nchi za ng’ambo kwenye malipo mazuri.

**Tanbihi**

Mtahini ahakiki hoja za watahiniwa.
Mtahini aoneshe pande zote mbili.
Kisha atoe msimamo wake.

**3. Baniani mbaya kiatu chake dawa.**

- Hii ni insha ya methali.
- Maana kiatu cha baniani ni kitu au kundi la watu linalochukia / kudharau kitu.
- Dawa: Kitu husika huenda kikawa ndicho jibu au jawabu suluhisho kwa tatizo fulani maishani mwa mtu katika jamii.

- Mtahiniwa aandike kisa kuthibitisha matumizi haya ya methali.
- Mtahiniwa azingatie pande zote mbili.
- Methali nyingine yenye maana sawa ni
  Matikiti na malango ndio maponya njaa.

**Utunzaji**

- Pande zote za methali zishughulikiwe.
- Anayeshughulikia upande mmoja asipite alama ya C /08/20
- Anayekosa kulenga katika kisa chake kimaudhui – apate alama D/03/20.

**4. Mtahiniwa alitimisha insha yake kwa maneno aliyopewa**

- Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa.
- Kisa kilenge tukio lililozua taharuki miongoni wa wahusika.
- Tukio lenyewe lazima lidhihirishe maafa / maangamizi.
- Tukio lenyewe litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba. katika gari n.k

**TB**

- Wanaofungua mlango wawe nje.
- Mtahiniwa atumie nafsi ya tatu hali ya wingi (warejelewa).
- Atumie wakati uliopita.